MAHUBIRI N°60: JUU YA MT.23:34-35

(*Ilihubiriwa kwanza kwa mwaka 2002 pa Locodjro, Abidjan - Côte d'Ivoire. tazama kaseti N°11 / www.matth25v6.org*)

Sasa wandugu, Roho kwa makusudi anaarifu kwamba nyoka… Je ! mumekwisha kusikia mlio wa nyoka? Wakati siku moja Yesu-Kristo alikuwa pale mbele ya mababu wa hizo nyoka… walimwambia Yesu: *"sababu gani unasema nasi kwa mifano ?"* Yesu aliwaambia : "*Inafaa yatimie maneno yote yaliyo andikwa juu yangu katika sheria ya Musa, na katika manabii, na katika zaburi*". Munaona? Ni katika Luka 24:44. Na zaburi 78:2 inasema: « *nitafungua kinywa changu kwa mifano, nitatangaza fumbo za nyakati za kale…* ». Walimwambia Yesu: *"Zaburi, ni nyimbo tu, huwezi kushika nyimbo kama msingi wako kwa ku…"*. Huu ni mlio wa nyoka! Lakini kwetu sisi, zaburi, maono, mifano ya Yesu hata maombolezo ya Yeremia ni Neno la Mungu kama vile haizuru shairi gani la Biblia. Japo, Mt.13:34-35 inasema kwamba Zab.78:2 ni unabii kuhusu Yesu. Na wajukuu wa wajukuu wa hizo nyoka watasimama mbele yenu kwa kusema: *"Lakini, Mat.25:6, ni mfano tu!"*. Huu ni mlio wa nyoka! Kwa mawazo yao, Yesu alipashwa kusema: *"Ndivyo asema Bwana, ufalme wa mbingu utafananishwa…"*. Lakini kwa kweli Mt.25:6 ni fumbo, ni mfano kwao lakini kwetu sisi ni utabiri. Yesu alisema: *"ufalme wa mbinguni uta…"* Munaona? Ni kwa wakati utakao kuja. Yesu alipokuwa akisema, Kanisa lilikuwa halija kuwa bado mchumba wake kwa sababu ni Paulo ndiye alifanya hii kazi. Paulo anasema hivi katika 2 Kor.11:2 : « *…kwa sababu niliwatayarisha ninyi kwa mume moja tu, kwa kuwaleta mbele ya Kristo kama bikira aliye safi* ». Munaona? Ni kwa ajili yao ndipo Yesu alisema kwa mfano kama inavyo andikwa katika Mt.13:10 kusudi uzao wa Kaina usifahamu ili pia mbegu yao ifunuliwe kama ilivyo kuwa kwa wakati wa Yesu. Kwa mfano, twajua kwamba mfano wa Mt.13:24-30 ni siri ya unabii ambayo Yesu alitafsiri toka shairi la 36 hadi shairi la 43 hata kufikia kusema kwamba mavuno ni mwisho wa nyakati, kwa kuonyesha kwamba ni utabiri utakao pata utimilifu wake katika siku za mwisho ijapo kwa mafikiri yenu ni mfano wa kawaida tu.… Ndiyo maana wandugu, kama inavyo andikwa katika Mt.16:5, mufanye angalisho kwa sumu na mlio wa uzao wa nyoka. Yesu hakuwatambulisha na kiumbe chengine ila tu nyoka kwani ni kile walicho, pia mlio wao unasikika tena. Munaona? Wafarisayo walikufa lakini roho zao ziko tena pale pembeni ya mambo Yesu iko akifanya. Amina! Hata kama Yesu angelisema katika Mt.25:1: *"Ninafikiri kwamba ufalme wa mbinguni utafananishwa…"*, mimi singeliona tofauti. Hata mawazo ya Yesu ni Neno [la Mungu]! Ningependa pia kusema asubuhi ya leo kwamba mifano ni utajiri wa kipekee wa masemi ya Afrika ya weusi na anaweza tu kusema: *"ni mfano bure"* mwafrika aliye poteza msingi wake wa kiafrika. Mtu bure! Mtoto haramu, aliye mwafrika tu kwa rangi ya ngozi. Nilizaliwa na niliishi kijijini na sikuona mwenye hekima wala mzee kusema pasipo mifano. Munaona? Wenye hekima watafahamu lakini waovu na wapumbavu hawata fahamu. Danieli 12:10 aliisema.

Vema, tushike Biblia zetu katika kitabu cha Mt.23:34-35 na baadaye nitasoma Yobu 33:23-24 ambayo nitazungumzia siku ijayo. Tusome katika Mt.23: *« Ndiyo maana, mimi, nitawatumia manabii, na wenye hekima, na waandishi ; na mutawauwa na mutawasulibisha, na mutawapiga mijeledikatika masunagogi yenu, na mutawatesa mji kwa mji, kwa namna ije juu yenu damu yote isiyo na kosa iliyo mwangika duniani, tangu damu ya Abeli mwenye haki, hadi damu ya Zakaria, mwana wa Baraki, ambaye mulimuua kati ya hekalu na mazabahu ».* Tusome pia Yobu 33:23-24: « *Ikiwa kwake kuna mjumbe, mwenye kutafsiri, mmoja kati ya elfu, kwa kumwonyesha mtu yaliyo sawa kwake, atamupa neema, na atasema: Umfungue ili asishuke katika shimo: nimepata upatanisho. »* Amina ! Mtafakari hii shairi la Yobu 33, nitarudilia mambo yale kama vile ninavyo rudia leo juu ya Mt.23.

Hakika nilisoma katika kitabu cha mtakatifu Mathayo lakini mtu wa kwanza ambaye ningependa nizungumzie hapa ni Henoka. Henoka aliishi kabla ya gharika. Katika kitabu cha Yuda shairi la 14 Biblia inasema kwamba alikuwa wa saba. Kwanza ni Adamu katika Mwanzo 5, kwa shairi la 1, shairi la 3 kuna Seti, shairi la 4 kuna Enoshi, wa nne ni Kenana kwa shairi la 5, wa tano ni Mahalaleeli kwa shairi la 12, wa sita ni Yeredi kwa shairi la 15 kisha wa saba ni Henoka. Huwezi kuzungumzia watumishi watakatifu wa Mungu pasipo kuzungumza juu ya Henoka. Mwa.5:24 inasema: « *na Henoka alitembea na Mungu ; na hakuwa tena, kwani Mungu alimuchukua* ». Ni kunyakuliwa ya kwanza inayotajwa katika Biblia.

Na huyo nabii akatabiri kwamba siku moja Mungu ataharibu dunia kwa maji. Utasema: *"Ndugu Filipo, je! Henoka alisema maneno haya?"* Ndio, Mungu aliifunulia dunia kupitia Henoka. Henoka alikuwa nuru ya dunia na huwezi kuokolewa au kuwa katika mapenzi ya Mungu ila tu kwa Henoka. Je! Huyo Henoka alikuwa ni nani? Yeye alikuwa mtu wa kwanza aliye tembea pamoja na roho ya Elia. Alikataa makanisa zote, miundo, na madhehebu ya wakati wake kwa kubaki na ufunuo wa Mungu. Hakutembea kwa mafundisho ya kanisa fulani lakini pamoja na Mungu. Ni pale Mungu alimchagua Elia. Munaona? Ni huyu Henoka ndiye alivaa ngozi ya nyama na ilibidi kumtambua katika Elia. Huyu mtu aliye panda mbinguni katika Mwa.5, ni Henoka. Huyu mtu aliye panda mbinguni katika 2 Wafalme2, ni Henoka. Na yule mtu atakaye panda mbinguni katika Ufu.11, ni Henoka. Henoka alipo ondoka duniani, hapo ni nuru iliondoka duniani kwani makanisa hayakuitaka, dunia haikupendezwa nayo... siku ile walipo ondoa Yesu duniani kwa kumuweka juu ya mti, dunia nzima ikavikwa giza kwani yeye alikuwa nuru ya dunia.

Na wakati ya utimilifu ya unabii huu ilipo fika, dunia ilijua kwamba itabidi Mungu aharibu dunia kwa maji. Na miundo zote za kidini zilipatana kwa kutumika katika hiyo hali kama ilivyo ufahamu yao ya unabii. Na walingojea kuchukuliwa kama vile Mungu aliifanya kwa Henoka ambaye wote walikuwa wakijidai kuwa wake baada ya kuchukuliwa kwake. Wakati ya huo unabii ilipo timia, hesabu ya watu duniani ilikuwa imefikia kati ya bilioni saba au nane. Kulikuweko makanisa mengi zaidi kuliko siku hizi. Kila chumba cha sinema kikageuka kuwa kanisa, na kulikuweko "*watu wa Mungu*", wakuu kuliko Osborn, Benny Hinn, Reinhard Bonnké na Yongi Cho. Shule kubwa kubwa za wachungaji kama vile *"Lemec Theological Institute"*, ya jina ya Lemeki, mjukuu wa Kaina na ndiye babu wa wateolojia, zilijaa duniani.

Kwa wakati wa Noa, wana wa Kaina waliweza kusema kwa furaha: *"sasa injili imeenea mipaka ya dunia na kwa neema ya Mungu, upendo, uvumilivu na upendo wa ndugu zimekaa kati yetu! Vizuizi vyote vimevunjwa. Hata pia kwa neema ya Mungu, mumethodisti anaweza kwenda kushiriki meza ya Bwana kwa wabatisti"*. Unaweza kusema, ndugu Filipo, unataka kusema kwamba wakati itakuja ambapo maneno haya yatafika? Ndio wandugu, watakwenda kushiriki meza ya Bwana wamoja kwa wengine! Na ni ile walifanya na hapo kwa wakati ule, bahati mbaya kwao, kama katika ndoto, Mungu akapandisha Noa. Maneno yale yatafika.

Noa hakufanya teolojia, hakuwa na masemi mazuri, hakuwa na elimu kama wachungaji wa wakati wake. Oh, sikujua hata kama nitaingizwa shuleni. Nilipo kuwa bado ningali mdogo, mume na muke wazee waliyokuwa matajiri na walikuwa tasa walipenda kunikubali kuwa mwana wao ili niriti mali mengi waliyo nayo. Nilipashwa kuwa na umri wa miaka mitano na niliona kwamba walishirikiana na wazazi wangu mara kwa mara. Kwa mwisho, sikukwenda. Lakini ningekwenda, inawezekana singeingizwa shuleni. Neema ya Mungu ikashinda umaskini ya wazazi wangu. Na kwa neema hiyo, ninajua kusoma na kuandika. Munaona?

Katika siku hizi ni elimu na mali ndivyo vinafanya mtu awe *"mtu wa Mungu"* na wanasema: *"zahabu na fedha ni vya Mungu"* lakini twajua kwamba Elia alivaa ngozi ya nyama, na Yoane mubatizaji, yule ambaye Yesu mwenyewe alisema kwamba ni mkuu zaidi kati ya wote waliyo zaliwa na mwanamke, alivaa ngozi ya nyama. Munaona? Hadi leo, sina motogari! Sina koti! Sina mwenyekiti! Lakini kama Noa, Elia na Yoane mimi pia nina kitu ambacho hawana: nuru ya wakati huu. Tayari wao ni katika utawala wao lakini utawala wetu sisi ni utawala utakao kuja. Munaona? Noa, Elia, Yoane na wengine, watu halisi wa Mungu walikuwa upweke kama Henoka, na walihukumu yote wengine walikuwa wakifanya. Noa hakuwa na cheti cha teolojia lakini alihukumu hata waliyo fwata ujumbe wa Henoka ambao yeye mwenyewe Noa aliamini kwanza na kuukubali. Hapo vita ikaanzishwa, vita ya wingi wa ukweli juu ya Ukweli moja, vita ambayo ilikomeshwa kwa garika. Munaona? Kilicho weka Noa kwa masitaki pamoja na watu wa kizazi chake ni kwa sababu alikuwa mwenyi kuhukumu, na alisema hazarani kwamba wao ni wachawi kuliko abaki kimya na kufanya kazi yake mwenyewe anapo jiweka kando. Waliona kwamba Noa aliwazarau watumishi wanao tumikia Mungu kwa kweli, Neno kubwa sana ni kwamba alijaribu kusema kwamba hakuna awezae kuokolewa ila tu kwa ujumbe wake. Alihubiri kwamba kusudi mtu yeyote aokolewe kutoka gharika, ilibidi tu kuamini maneno aliyo kuwa akiyasema na kuja katika safina. Alihubiri kwamba hakuna awezaye kuwa katika mapenzi ya Mungu ila tu kwa ujumbe wake. Watu walimwambia kwa kumzihaki: *"Noa, unataka kusema kwamba Adamu na Henoka, babu zetu ambao hawakukuamini wewe watakwenda katika Gehena?"* Munaona ? kwa ufahamu wao, maneno ambayo Noa alisema siyo ya kusikika kwa mutu mwenyi akili ndio maana hayakuwaogopesha. Lakini Noa alisema: *"Adamu na Henoka watahukumiwa pamoja na vizazi vyao, lakini kizazi hiki kitahukumiwa kwa ujumbe wangu na kama ninyi ni uzao wa Adamu wala wa Henoka, mutasema amina kwa kila moja ya maneno yangu na mutakuja katika hii safina"*. Na walianza kucheka kwa namna Noa na nyumba yake ndogo walipata haya. Ijapo wakati ule, hakuweko Biblia na hapo Mungu alisema na kizazi teule kama alivyo sema na Adamu katika Edeni. Na Noa siku moja aliweza kuona katika roho: tai akiruka katika mbingu. Tai iliangalia juu ya kisiwa na tazama palikuwa umati wa kuku usiyo weza kuhesabika na hesabu yao ilikuwa kama nyota za mbingu na tai akawapigia kelele na kusema: *"Inabaki siku 40 samaki za bahari zitaogelea juu ya hiki kisiwa! Rukeni zenu na muje pamoja nami milimani!"* na kuku wakajibu wote pamoja: *"Tunakataa, ni uwongo!"*. Na wakati Noa alikuwa akiangalia, tazama, kiwango cha maji kiliongezeka na kuku walilia, waliruka ruka. Na tayari, kisiwa chote, kuku na miti vilishuka katika kilindi cha maji. Na maono yakaacha roho yake na Noa akasema ndani mwake: *"Basi kama hao kuku wangeamini, namna gani wangeweza kuruka?"*. Mungu akaonyesha Noa kwamba si kwa sababu hao wachungaji hawapendi kuamini lakini kwamba ndani mwao wenyewe, hakuna namna waamini au inayoweza… Munaona? Hata kama wangependa kuamini, haingewezekana. Ni kama vile ungeingia porini na kutafuta mti unao weza kutoa damu. Ni kama vile mtu anakuomba kitu ambacho huna. Ni kama vile muefraimu anaombwa kusema « *Shiboleti* ». [*Kusanyiko wanasema: Amina!"*]. Munaona? Na Noa alipo ingia katika safina, Mungu akaacha muda upite kiisha, Mungu mwenyewe akafunga lango la safina. Munaona? Mjumbe anapo aga dunia, [hapo] njia ya mbinguni inaanza kufungamana kama piramidi hadi kuvutika kisha mara tena, Mungu anapandisha kizazi chengine cha watu na kutuma mjumbe mwingine. Munaona?

Tena, baada ya Noa, kukawa mtu mmoja na jina lake ni Musa. Kujulikana kwake kulitokea tu kwa neema ya Mungu. Katika ukuu wa uungu, juu ya uso wa dunia, Mungu akamwangalia na kumjalia neema. Hakuwa na hekima, akili na kujulikana kama Kore na Datani lakini alikuwa kinywa cha Mungu. Kama Musa angesema twendeni kushoto, haizuru miujiza na maajabu gani Kore, Datani na Abiramu watafanya kwa kusema kwamba inafaa kwenda kuume, ulilazimishwa kwenda kushoto pamoja na Musa. Hata kama watu wote wanakwenda upande wao, nenda zako kwa upande wa Musa. Na katika kitabu cha Hesabu 16, mia za watu, wale wasiyo jua kwamba juu ya uso wa ulimwengu yote Mungu anasema kupitia mtu moja tu waliangamizwa. Munaona? Kwa utofauti na wayahudi, watu wa mataifa hawazoei manabii ndio maana wanapenda wamuelewi nabii kiakili. Kila mara Viongozi wao ni wafalme, watawala, watu wanao waongoza kwa hekima yao. Na ni aina ya mchungaji. Munaona? Sababu iliyo waleta wayahudi kumsumbua Yesu [kwa maulizo], ni kwa sababu wanajua kwamba kumkataa nabii ni kumkataa Mungu. Lakini mataifa hawajui hata nabii ni nani, namna gani watajisumbusha? Myahudi anajua kwamba kuhani wa kweli [mchungaji] ana uwezo tu wa kulinda imani ya taifa lakini ni nabii peke ndiye anajua mapenzi ya Mungu…

Vema,… kulikuwa watu, watu,… na kukawa Yeremia. Lakini kabla ya Yeremia, kulikuwa Uria. Katika utoto wake na ujana wake, Uria alipo kwenda katika masinagogi, macho yake yaliona tu makuhani wakuu, wanao agopa Mungu… lakini wakati Yule aliye mzania kuwa Mungu ambaye wale makuhani na manabii walitumikia alipo mwita, kukawa vita. Vita ya Ukweli na uwongo ikaanza na mwisho wa hiyo vita ilikuwa kifo chake. Rehema! Basi Uria alifanya nini? Tusome Yeremia 26:15-23 « [na Yeremia akawaambia]: *lakini tu, mufahamu vizuri ya kwamba, kama munaniua, mutaweka damu isiyo na kosa juu yenu, na juu ya huu mji, na juu ya wakaaji wake; kwani kweli kabisa Bwana alinituma kwenu ili niseme masikioni mwenu maneno yote haya. Na wakuu, na watu wote wakawaambia makuhani na manabii: mtu huyu hastahili kufa; kwani alisema nasi kwa jina la Bwana wa Milele, Mungu wetu.*

Na watu wamoja wamoja wa wazee wa inchi wakasimama, na wakasema na makutano ya watu wakisema: Mika, mumorashiti, alitabiri katika siku za Ezekia, mfalme wa Yuda, na… Ezekia, mfalme wa Yuda, na Yuda yote pamoja naye basi wakamuua. Na tutafanya ubaya mkuu juu ya nafsi zetu. Na kulikuwa pia mtu ambaye alitabiri kwa jina la Bwana wa Milele, Uria, mwana wa Shemahia, wa Kiriathi-Jearimu; na alitabiri juu ya mji huu na juu ya nchi hii, sawa sawa na maneno yote ya Yeremia ; na mfalme Yehoiakimu, na watu wake wote wenye nguvu na wakuu wa inchi wote wakasikia maneno haya, na mfalme akatafuta kumuua ; lakini Uria akasikia, na akaogopa, na kukimbia, na akakwenda Misri. Na mfalme Yehoiakimu akatuma watu Misri, Elinatani, mwana wa Akibori, na watu pamoja naye, kule Misri na wakamuondoa Uria nje ya Misri, na wakamuleta kwa mfalme Yehoiakimu, na akamupiga kwa upanga, na akatupa mwili wake katika kaburi za wana wa watu. Munaona? Alipo kimbia, wasiyo amini waliweza kusema: *"Hukusema kwamba ni Mungu alikutuma, kwa nini unakimbia kwenda Misri?"*. Na kuhusu Yeremia Biblia inasema kwamba sasa ni wakuu wa inchi na watu ndio wanasimama na kuwaambia makuhani na manabii wasimuue Yeremia. Munaona? Kwa upande moja kuna umati wa makuhani na manabii lakini kwa upande mwingine, ni Yeremia anaye washambulia… Makuhani, wanao shika gombo za Musa mikononi mwao, na manabii wanao jizania kuzungumziwa na Mungu, wanataka kumuua Yeremia. Munaona kwamba si yule yule Mungu wa Yeremia ndiye anaye waongoza na si yeye anaye sema na hao manabii? Sasa, tazameni mambo haya! Taifa lilianza kutambua: Noa alikuwa pekee juu ya wote ni yeye alisema kweli. Mika, mumorashi alikuwa peke juu ya wote na alitambulika kuwa mwenyi haki wakati muda ulikuwa umepita. Wakakumbuka tena kwamba Uria, mwana wa Shemahia alikuwa peke juu ya wote na alitambulika kuwa mwenye haki muda ulipo pita. Elia alikuwa peke juu ya wote na ni yeye

aliye sema kweli. Munaona? Amosi alikuwa peke juu ya wote na maneno yake yalikuwa kweli. Munaona? Taifa likaanza kufanya angalisho! Munaona? Isaya alikuwa peke juu ya wote na alikuwa wa kweli. Taifa likawaambia makuhani na manabii: Hapana! Mara hiyo inabidi tuone vizuri! Kila mara kuna mtu moja anaye pingana nasi wote na baada ya kufa kwake tunaona kwamba alisema kweli, mara hii, inabidi tuangalie vizuri! [*Kusanyiko linasema: Amina!*].

Tuchukue Yerermia sura 26:7-8. Tuisome: « Na makuhani *na manabii na watu wote wakamsikia Yeremia akisema maneno haya nyumbani mwa Bwana wa milele. Na ikafika, wakati Yeremia alipo maliza kusema maneno ambayo Bwana wa Milele aliamuru kuwaambia watu wote, makuhani na manabii na watu wote wakamshika, wakasema: Hakika utakufa!».* Munaona tena? Tupapo ona kwa historia kwamba nabii Isaya alikatwa vipande vipande, tunafahamu kwamba mamlaka ya kutokurudi nyuma mbele ya uzao wa Kaina ni kwa Mungu peke. Yeremia anapo fikia hatua ya kulia kama inavyo elezwa katika Yer.20:14-18, wakati kuhani mkuu Pashkhur alimpiga kofi na kumuweka gerezani, wakati katika Yer.38:7, wale wale wachungaji na manabii walimshusha Yeremia shimoni, namna gani yule ambaye haku ahidiwa na Mungu kwa kazi kama hii anaweza kusimama imara? Namna gani makanisa zaweza kukubariki? Munaona?

Baada ya haya, nabii Elia. Na ile ile vita ikaanza, kupiganisha roho ya makosa na kuchukuliwa kwa Elia ikawa mwisho wa vita hiyo. Alikuwa peke juu ya makuhani, manabii na watu kwa wakati wake. Mutaona kwamba katika 1 Wafalme 18, hakuweko hata nabii moja mwingine kwa upande wake na katika 1Wafalme 19:10, alisema: *«Nilikuwa mwenye wivu kwa Bwana wa milele, Mungu wa Majeshi; kwani wana wa Israeli wameliacha agano* lako*; wamepindua mazabahu yako na wamewaua manabii wako kwa upanga, na nimebaki, mimi peke, na [sasa] wanatafuta maisha yangu ili waiondoe ».* Lakini wao waliona kwamba hao ni manabii waasi na wenye kukosa adabu kama Elia, waliwaua hao manabii kufwatana na yale Musa aliwaagiza. Zamiri yao haikuwasitaki hata kidogo.

Baada ya Elia, ningependa niseme juu ya Mika mwana wa Jimla katika 1 Wafalme 22. Kwa wakati ule, kulikuwa manabii mia ine wakuu katika Israeli. Manabii wa kimo cha Billy Graham, Ewald Frank, Ushe Praise, Osborn et Yonggi Cho. Kwa muda mfupi, walikutana. Walijuana, walizoea kutembeleana na mara walifanya mikutano pamoja. Walikuwa wandugu katika kristo ijapokuwa mafundisho yao ni tofauti. Lakini Mika alikuwa peke na wakati alikuja, alikuwa peke. Pia katika 1 Wafalme 22:24, Mika alimwambia Ahaba: *"Na sasa, tazama, Bwana wa milele ameweka roho ya uongo kinywani mwa manabii wako wote ambao ni hawa, na Bwana wa milele ametamka mabaya juu yako*". Na Sedekia, moja wa manabii, akakaribia na kumpiga Mika kwa shavu, na kusema: *"Ni kwa njia gani alipita Roho ya Bwana wa milele, mbali nami, kwa kusema nawe?"* Na tunajua kwamba Mika alikwenda gerezani kwa ajili ya maneno yale na vita hiyo ilipashwa kumalizika kwa kifo chake.

Kisha Mungu akamtuma Amosi, tuisome katika Amosi 7:10: « *Basi Amazia, kuhani wa Beteli, akatuma kwa Yeroboamu, mfalme wa Israeli, akisema: Amosi alikusudia kukuua kati ya nyumba ya Israeli; inchi haiwezi kuvumilia masemi yake yote».* Shairi la 11 inasema: « *Na Amazia akamwambia Amosi: Muonaji, nenda zako, Ukimbilie inchi ya Yuda, na huko, ule mkate, na utabiri kule, lakini usitabiri tena hapa Beteli, kwani ni mahali pa utakaso wa mfalme na pia nyumba ya ufalme. Na Amosi akajibu akamwambia Amazia: mimi sikuwa Nabii, wala sikuwa mwana wa nabii; lakini nilipokuwa nikichunga ufugo, na nilipokuwa nikichima matunda ya mkuyu na Bwana wa milele alinitwaa nilipo kuwa nikilisha wanyama, na Bwana wa milele akaniambia: kwenda, utabiri juu ya Israeli taifa langu.».* Munaona? Sikuwa nabii wala mwana wa nabii, sikujua lolote kuhusu Mungu lakini tarehe 24 aprili 1993, niliitwa na kutumwa kwa kutimiza kazi kama alivyo andika Mt.25:6 na Ufu.12:14. Munaona? Elisa angeweza kusema: sikuwa nabii wala mwana wa nabii lakini nilikuwa nikilima shamba langu na kura ya Bwana wa milele ikaniangukia. Mtu wa kiroho sana, kuhani mkuu wa Betheli anamfukuza Nabii Amosi, anapo kubaliwa na taifa pamoja na mfalme. Rehema! Angalieni lile analo lisema na mutaona kwamba ni maneno ambayo tunazidi kuishi. Alisema: *« …inchi haiwezi kuvumilia masemi yake yote »…*

Kinacho tufurahisha ni kwamba kinacho toka kwa Mungu kila mara kina ushindi na pia Kelele ya katikati ya usiku itashinda. Ginsi vile huwezi kusimamisha tetemeko la inchi ndivyo huta weza kusimamisha Ujumbe huu wa unabii unao kuja kwa kuenea dunia nzima…

Kisha Mungu akatuma Yoane mubatizaji. Baba yake alikuwa kuhani lakini akakwenda zake jangwani ili asije kupokea lolote kutoka kwake. Ni Mungu aliye mtuma, hakuwa na lolote la kupata toka mtu. Munaona? Je! Mjumbe wa wakati anafanya nini! Anawahamakia makuhani wote. Lakini ginsi Mungu hapandishi wajumbe wawili kwa wakati moja, ilibidi Yoane Mubatizaji aondoshwe kazini ili amwachie Bwana Yesu [nafasi]. Na ilifanyika hivi. Kisha Bwana akaanza kuongoza Israeli kwa gongo la chuma. Lakini makuhani, wafarisayo, wasadukayo, waesenia, waliona mambo kwa namna ingine. Kwa mafikuri yao, kama Yesu anaona kwamba wao ni katika makosa, ni lazima ajenge sinagogi lake na atabiri kwa wale wanao taka kumusikiliza na kule mbinguni tutaona ni nani aliye wa kweli ao wa uwongo. Lakini Yesu hakuwa na maoni kama haya. Alijua kwamba yeye alikuwa nuru ya dunia na ni yeye peke alikuwa na Kweli, na msimamo wake ulikuwa ni kwenda hadi mwisho katika vita ambayo mwisho yake inajulikana ni kusema kufa kwa mjumbe. Kisha mwishowe, akajikuta peke juu ya wote. Peke juu ya watu wote. Peke juu ya Herode. Peke juu ya Pilato. Na Yoane 9:22 inasema kwamba: « *…wayahudi walipatana kwamba ikiwa mtu atamkiri kuwa Kristo, atafukuzwa toka sinagogi ».* Munaona? Wale wale wana wa shetani ni pale. Hawasemi kitu kwani wanasemezana kwamba wakisema [mabaya] juu ya Kelele ya katikati ya Usiku, wataitangaza pasipo kupenda na kuileta ijulikane na watu wengi. Lakini watafikia kuwapa watu angalisho juu ya kitabu hiki cha kimajani. Tazama, mumearifiwa. Wamoja wataisoma kwa kutafuta ujuzi ijapo wengine hawata izungumzia kwa uangalifu kwani wanasema kwamba jambo lile linaweza kuwa linatoka kwa Mungu. Lakini mufahamu kwamba wale wote ni watoto wa shetani. Yesu alipo kuwa akihubiri, walisema katika sinagogi yao… Wandugu, walialika mkuu zaidi wa dini, mteolojia mkuu mbele ya Bwana wa milele na siku ile, katika kanzu yenyi kungaa na ndevu zake ndefu, baada ya kusoma katika gombo la Musa, akasema: *"Huyo Yesu ni mdanganyifu kwani maandiko yanasema kwamba Masiya atakuwa mchungaji wa Israeli, kuhani mkuu Melkisedeki japo ni lazima makuhani watoke katika kabila la Lawi lakini huyu Yesu ni wa kabila la Yuda na mambo haya hayaambatane na maneno yaliyo semwa na Musa. Wafwasi wake wanakula pasipo kunawa mikono, hawaheshimu sabato. Kwanza hasemi maneno mazuri isipokuwa tu kuonyesha ubaya na uzaifu wa makanisa [zingine] kwa kuwadanganya wazaifu lakini Mungu abarikiwe, sisi ni katika maandiko! Alleluya!!!…* [*Amina!!*] *anapenda kuongoza watu wote kwake tu, ijapo, ambacho Mungu anatuomba ni kushika sheria ya Musa!!! Na haya, yaweza kufanyika toka mahali kote, haizuru sinagogi gani, uwe mufarisayo, musadukayo, esenia, muyunani ao muherodia. Utofauti wa mafundisho si kitu!!! Ya lazima, ni Yesu, ni kuishi vizuri!!! Ni kama watu weusi, wa kimanjano, wazungu. Mbinguni, kutakuwa rangi moja!!! Sisi ni shamba la mboga ya Mungu inayo maua mbalimbali !!! Aleluya!... sisi ni wa Musa!!! Musa tu !!! Musa alisema yote!!! Musa alifunua yote!!! …".* Ndugu

[zangu], baada ya saa moja ya mahubiri, ilikuwa ajabu. Walibariki Mungu kwa sababu hawakufwata Yesu-Kristo na wakaomba ili Mungu awakomboe wale waliyo danganywa na Yesu-Kristo, hii ilikuwa ni maoni yao. Na leo watafanya tena hivi. Lakini najibu pia na kusema kwamba ninyi ni shamba la mboga la Ahaba na kwamba kwa sababu ya shamba hilo mulimuua Naboti, manabii pia mulimuua Yesu-Kristo na sasa munatafuta kusulibisha ujumbe huu. Ni shamba la damu na la laana! Ni kwa shamba hilo wabranhamisti waliharibu ujumbe ya William Branham.

Munaona? Katika ujumbe ya huyo Shetani kuna mapepo mengi na pepo wa mwisho ni: *"Musa alifunua yote!"* ni pepo wa kale! Paulo alipo jiweka kama nabii, yule pepo wa kale alisema: *"Yesu alifunua mambo yote!"* William Branham alipo kuwa akihubiri, yule yule ibilisi alisema: *"yote imefunuliwa katika Biblia!"* Na wakati Kelele ya katikati ya usiku inapiga, yule yule pepo wa kale atasema kwa uzao wa nyoka: *"Branham alifunua yote!"*. Ni lazima waiseme kwani mababu zao pia walisema hivi. Maneno yale ni katika damu yao. Munaona? Ninataja damu ya nyoka inayo tambaa porini! Sawa sawa kuna kundi mbali mbali ya damu na rhesus mbalimbali, ndivyo kuna utofauti ya umati kati ya wale wasiyo weza kuamini ujumbe huu na sisi. Ijapo kweli, je! Musa hakufunua yote? Hakika! Lakini Mungu akawa tuma manabii!... munaona? Je! Paulo hakufunua yote hadi ginsi gani kuchukuliwa itaweza kufanyika kama inavyo andikwa katika 1 Thes.4:16-18? Na Paulo hakuwaambia watu wafarijike na maneno haya mpaka Bwana atakapo rudi? Ilitokea wapi Mungu awatume Wesley, Lutheri na Branham na inatokea wapi kusema kwamba Mungu hawezi tena kutuma mjumbe? Munaona?

Lakini jambo la ajabu, ujumbe wa Yesu ulianza kuvuma na adui zake walipoona kwamba faida yao inasongwa, wakafanya shauri. Munaona? Ijapo aliyosema ilikuwa kweli kwa msingi wa ufunuo ya unabii ambayo juu yake tayari lilikuwa limejengwa wokovu siyo tangu Mt.16:18 lakini tangu kabla dunia kuwekwa msingi. Ijapo, hata ikiwa maneno Yesu alikuwa akisema hayakupatana na yale Musa alisema, ni lazima kuamini! Hata kama wanafunzi hawanawi mikono mbele ya kula, inabidi kuamini! Hata kama Yesu haheshimu sabato, inafaa tu kuamini!...

Hata Biblia inatueleza kwamba makuhani ndio waliwasukuma watu kuchagua Baraba! Tusome Mt.27:20: *«Lakini wakuu wa makuhani na wazee wakawaambia wamuombe Baraba na kutolea Yesu auawe»*. Munaona? Hakika ni kama siku za manabii wote. Na sasa ni wachungaji na manabii ambao watawapa watu angalisho juu ya kitabu hiki cha kimajani. Munaona? Pia Yesu Kristo alitabiri katika Mt.23:34-35 kwamba atawatuma tena manabii ambao watakuwa na ukweli hapa duniani na watu wa dini watawakataa na kuwatesa. Kusudi wawajengee minara baada ya kufa kwao. Sasa turudilie Mt.23 kwa kumaliza: *«Ndio maana tazama, mimi, ninawatumia manabii, na wenye hekima, na waandishi ; na mutawaua na mutawasulibisha, na mutawapiga mijeledikatika masinagogi yenu, na mutawatesa katika kila mji, ili iwe juu yenu damu ya wenye haki wote iliyo mwangika duniani, tangu damu ya Abeli mwenye haki, hadi damu ya Zakaria, mwana wa Baraki, ambaye mulimuua kati ya hekalu na mazabahu.»*

Vema, Bwana anasema nini? *Niliwatumia manabii?* Hapana! Lakini *ninawatumia,* kwa wakati utakao kuja, manabii! *Muliwaua?* Hapana! Lakini… "*Mutawaua na mutawasulibisha, na mutawapiga mijeledikatika masinagogi yenu, na mutawatesa mji kwa mji*". Yesu Kristo atawatuma manabii duniani, manabii kama wale wa Agano la Kale. Maana ya nabii ni nini? Kutoka kwa kiebrania, neno *Nabia* maana yake ni *"mjumbe"*. Kwa uwingi ni *Nebiim* maana yake: *"wajumbe"*. Siyo wenyi upako au wanao miujiza lakini mjumbe! Kwanza nabii ni mwenyi kubeba ujumbe wa Mungu kwa binadamu. Na Mungu anapo tuma nabii mjumbe, ni kusema hakuna tena Ukweli duniani. Na anasema, anahukumu na pia anatamka hukumu ya Mungu, kwa mamlaka moja tu ambayo ni ya Mungu peke. Hakuna Ukweli au wokovu ila kwake tu. Hakuna awezaye kutumikia Mungu ila akiwa tu pamoja naye. Na Mungu anathibitisha ujumbe wake kwa alama na miujiza. Na kama yeye ni wa Kweli halafu ulimwengu wa kidini utamkataa. Na atakuwa peke juu ya wote. Sababu gani? Kwani anakuwa hatari kwa faida na mamlaka ya watu wengi. Hakuna awezae kumwamini pasipo kupoteza kwanza kwa muda sehemu ya kile alicho kuwa. Munaona ndugu Oskar anayekaa pale, imepita miezi mitatu, yeye alikuwa mchungaji wa pili katika kanisa moja. Ndugu Akobe na wengine wengi zaidi. Wao waliyo kuwa wachungaji, watakuwa waamini wa kawaida? Siyo rahisi lakini yasiyo wezekana kwa wana wa shetani yawezekana kwa wana wa Mungu. Munaona? Hao wachungaji na manabii pamoja na jamaa zao, wanao lishwa na kupangishwa na makanisa watafanya nini? Munaona?

Kama mtu anajidai kuwa nabii na anakwenda kujiunga na manabii wengine katika maseminari, mikutano, kimbia, ni mbwa-mwitu! Sasa sikilizeni: kondoo aliyekwenda mbali na zizi lake aliwaachia maagizo watoto wake akasema: *"Fungeni lango na mulale na mutafungua tu nitakapo rudi!"*. Nao wakasema: *"Mama, tunaelewa lakini tunakusihi utuletee majani mengi utakapo rudi!"*… Akawanusa kwa upendo kubwa na akakwenda zake. Hapo, mbwa-mwitu aliye kuwa kando akijificha akakaribia na kusema: *"Oh! Tayari mumelala? Fungueni lango mimi ni mwana kondoo kama nyinyi, ninatumwa na mama wenu ili niwaletee majani muliyo omba. Mfungue mlango!"*. Wana kondoo wakaangaliana na kusema: *"Wewe ni moja wetu?"* mbwa mwitu akajibu: *"Mimi ni moja wenu, munifungulie na mutaona rangi yeupe ya manyoya yangu na…"* Kisha moja wa wale wana kondoo akapata hekima ya kutazama chini ya lango na sasa aliona nini? Hakuona kwato lakini miguu ya mbwa-mwitu yaliyo na kucha zikaonekana kidogo kidogo ndani ya ngozi kubwa ya kondoo. Na akapaza sauti: *"Ni mbwa mwitu! Tazama miguu yake chini ya lango!"* na mbwa mwitu alipoona kwambwa ametambulika, akakimbia. Munaona? Ni kweli tunahitaji majani ni kusema miujiza na Neno lakini tufahamu kwamba tutagonjwa tena na hata kufariki. Tusitolee nafsi zetu kwa miujiza ya udanganyifu. Yesu Kristo anapenda kanisa lenyi hekima kama inavyo andikwa katika Mt.25 kwani yeye mwenyewe ni ukamilifu wa hekima. Kufwatana na yote tulishika kutoka Noa, Yeremia, Elia na kutoka manabii wa kweli wa Mungu, tangu wakati nabii anapo karibia na kusema kwamba alifwata mafunzo ya teolojia, yeye ni mbwa-mwitu! Wakati nabii anapo karibia pasipo ujumbe ambayo ni nuru kwa kizazi chake lakini anakuja na kanisa moja, huduma, misioni au maneno ya ujuzi, huyo ni mbwa-mwitu! Anapashwa kuja na ujumbe utakao fungua macho ya wateule. Neno la Mungu linamjia tu nabii na huyo anawajia watu na Neno kwani katika mwanzo lilikuwa Neno na kama sisi ni watoto alisi wa Mungu, tulitoka kialisi katika Neno, tutaamini hata kama watu wote wataikataa. Neno Kanisa ni muungano ya wote waliyo toka katika makanisa kwa kukusanyika kando ya ujumbe ya wakati wao. Munaona? Wakati nabii anaonekana na anaanza kushirikiana na nabii mwingine ijapo waliunda makanisa, misioni au huduma tofauti, hao ni mbwa-mwitu na musikose kuwaambia kwamba ni roho ya chatu inayo waongoza. Wakati mtu anakaribia na anajidai kuwa nabii, mumuulize wito wake, kutumwa na ni wapi katika Biblia Mungu alisema kwambamtu atakuja kutimiza kile anacho fanya. Kwa mfano: Isaya 40:3 ilitangaza kwamba Yoane mubatizaji atakuja na yeye mwenyewe aliisema katika Mt.3:1-3. Isaya 61 ilitanguliza Yesu na Yesu aliisema katika Luka… sura ya ngapi? [ndugu mmoja anasema: Luka 4:16-21]. Luka 4… Asante ndugu! Na Isaya 49:6 ilisema kuhusu Paulo ilipo sema « *Nilikuweka uwe nuru kwa mataifa, ili uwe kwa wokovu hadi mipaka ya dunia»* na Paulo aliisema katika Matendo 13:47…

Na kwa kumaliza, ningependa niseme hivi: kila mtu anakubali, hata Ewald Frank, kwamba tuko usiku wa manane na William Branham kwa mwisho wa huduma yake alisema kwamba tuko kwa usiku wa manane kosa dakika. Namna gani miaka arobaini baada ya William Branham, hatuta kuwa kwa usiku wa manane? Munaona? Na kwa msingi wa Danieli 12, hamuhitaji Mt.25:6 kwa kuamini. Kwa msingi moja tu ya Ufu.12:14, hamuhitaji Mt.25:6 kwa kuamini kwamba kunapashwa kuwa Kelele ya Usiku wa manane. Munaona? Kwa wakati wa jioni, Shetani alisema kwamba nguzo la wingu ni wingu la kawaida huko Tukson na kama hapo saa sita manane, anakuambia kwamba Mt.25:6 ni mfano bure, mumuonyeshe yale. Mumuonyeshe Yosua 6, mumuonyeshe 1 Wafalme 19, mumuonyeshe Esitheri! Mumuonyeshe Isaya 30. Mumuonyeshe Biblia yote! [*Kusanyiko wanasema: Amina!*].

Sasa, tambua kwamba katika ono, William Branham alipokelewa kati ya waliyo wake. Iliyo pashwa kufika anapo kufa, Mungu akamuruhusu kuiona. Lakini kumbuka kwamba William Branham hakuona Musa, hakuona wala Yeremia, wala Paulo, wala Lutheri, wala Wesley. Munaona? Kila mjumbe alikuwa pamoja na kundi lake. Mjumbe anaporudi, Mungu anafunga mlango kwa sababu wakati ya neema kwa kizazi kile inapunguka na kumalizika na hapo giza inaingia tena. Munaona? Noa alipo rudi katika safina, kukawekwa siku saba ya muda wa neema! Lakini sivyo kila mara kwani, Musa alipo rudi katika kundi lake, [hapo hapo] mlango ukafungwa. Musa alipo rudi baada ya huduma yake, mlango ulifungwa juu ya Musa na kundi lake. Na tangu Yosua, hakuna aliye weza tena kuingia pamoja na Musa. Huu ni ufunuo wa kweli. Wote walio kuja baadaye, Musa aliwaambiya wakwende kwa yule aliyekuwa akiuza mafuta baada yake maana yake kwa Yosua. Kila mara duniani Mungu ana mtu moja ambaye inabidi mumwamini kama inavyo andikwa katika Yoane 6:28. Kazi na mapenzi ya Mungu ni kumwamini yule aliye tumwa na Mungu.

Kule walimwambia William Branham: *"Paulo ni pamoja na kundi lake! Utakapo maliza kazi yako, utapokelewa kwetu na utahukumiwa sawa sawa na maneno uliyo yahubiri…".* Na Paulo atakapo kuja, hatasema mambo aliyo fanya alipo kuwa chini ya sheria lakini kwake yote yataanza siku ile nuru ilipo ngaa pale njiani Damasiki na ile sauti ikamzungumzia. Na ikiwa ile sauti ya Mdo.9 ni sauti ya Mungu halafu ni heri kwa wote waliyo mfwata, na ole kwa wote ambao hawakumfwata. Munaona? Paulo atakuja na kundi lake. Atasimama na kusema: *"Bwana, uliniita katika ono kufwatana na kazi ya Isaya 49:6 na maneno niliyohubiri nilipewa nawe… ".* Kama Mungu hakubali Paulo ilikuwa ni mwisho kwa wote waliyo mfwata Paulo. Musa atakapo simama mbele ya kiti cha hukumu ya kiti cha enzi cheupe, atasema: "*Bwana, siku moja tulipo kuwa bado tungali Misri, malaika aliniita toka kijiti kinacho waka na alinituma…*". Na wote watakaribia: Martin Luther,… Kalvini,... John Wesley,… na sasa tunaona walutheri wanapokuja. Walisema: "*Sisi pia tuliamini Lutheri, mtumishi wako mtakatifu!*" Lakini Lutheri akapaza sauti: *"Mimi!! Sikuwajua wakati wowote!! Muliniona wapi? Muliamini kwa mwaka gani?"* Wakasema: *"Kwa mwaka 1560"*. Lutheri akasema: *"Kwa mwaka 1560, ni Kalvini! Muwapeleke kwa Kalvini"* [kusanyiko wanasema: Amina!]. Lakini Kalvini akasema: *"walijiita walutheri nilipo kuwa nikihubiri"* na Kalvini akawarudisha kwa Lutheri naye akawahukumu. Katika Luka 23:7 na 11: *Pilato alipo sikia kwamba Yesu ni wa utawala wa Herode akamurudisha kwa Herode.* Je! Itakuwa vipi kwa hukumu ya kiti cha enzi cheupe? Kwanza wafarisayo walikuja na kuliko [wamuone] Musa, wakaona Yesu. Wakashikwa na woga na kusema: *"Sisi ni wafwasi wa Musa!"* Munaona? Ndivyo walimwambia Yesu katika Yne.9:28. Na Yesu akasema: "*Kama ni vile, muwapeleke kwa Musa".* Munaona? Musa aliwauliza: *"Je! Mulikuwa jangwani? Kore na Datani walipo asi, je! Ninyi mulikuwa upande wangu? Munamujua Haruni na Miriamu?"* Walisema: *"Hapana!"*. Musa alishangaa na kusema: *"Basi mulikuwa nami huko Misri ila tu hamukutoka?"* Walisema: *"Hapana! Tuliishi duniani kwa mwaka 30, au 40 pale! Lakini sisi tulikuwa waaminifu kwako, sisi ni wafwasi wako!"* Musa akasema: *"Kwa mwaka 30, pale ni Yesu! Lakini!! Sababu gani basi munasema kwamba ninyi ni wangu?...Je! sikuwaambia kwamba Bwana Mungu wenu atainua kati yenu mtumishi kama mimi? Nendeni basi kwa Yesu!"* Walisema: *"Msamahani, Musa, usitufanyie hivi! Tulikutetea duniani! Basi tunakusihi utukubali kwako!* [Kusanyiko wanasema: Amina!!]. Munaona? Walipo sikia jina la Yesu, roho yao ikavunjika! Wakapata baridi. Wakakumbuka kwamba Yesu aliwaambia katika Yne.5:45: « *Musifikiri kwamba mimi, nitwasitaki mbele ya Baba; kuna yule anaye wasitaki, Musa ambaye munamtumainia ».* [*Kusanyiko wanasema: Amina!*]. Tunajua ya kwamba Neno la Mungu ni hukumu kwa wana wa shetani na wanapo sema: *"Sisi ni wa Musa!"*, wanapo mtaja mtu ambaye tayari amefariki, ni kusema wameshindwa kwa uamzi wa kwanza, ambao ni uamzi ya waliyo hai. Sisi ni wa mtu fulani au fulani ambaye tayari amefariki! Munaona? Wafarisayo walipo omba wapelekwe mbele ya Musa, walisikiwa lakini Yesu aliwaambia kwamba Musa atawahukumu. Basi kwa kufupisha yote, Mungu alitayarisha hukumu ya kiti cha enzi cheupe ambacho ni mfano wa baraza kuu ya wayahudi, mfano wa korti kuu yetu hapa, korti ya mwisho, ninafikiri. Munaona? Kusudi wasimkubali Yesu, wali jiandika juu ya hesabu ya wafwasi wa Musa. Walisema katika Yoane 9:28: *"… sisi ni wafwasi wa Musa"*. Namna gani munaweza kuwa wanafunzi wa yule ambaye hamukumjua naye hakuishi katika kizazi moja nanyi? Japo baada ya Musa, Baruku alikuwa mfwasi wa Yeremia, na Elisa alikuwa mfwasi wa Elia. Munaona? Na nyuma ya zaidi ya miaka elfu, walijifanya wafwasi wa Musa kusudi wasimkubali Yesu-Kristo, nuru ya wakati yao. Na sasa leo, wajukuu wa hao wafarisayo, ambao jehanama inawangojea, wameongeza na tena wanazidi kuongeza hesabu ya mitume na wafwasi wa Yesu. Leo kwa mwaka 2005, wao ni wafwasi, pia mitume wa yule mnazareti aliye tembea katika barabara za Yerusalema yeye ambaye alikuwa na mitume kumi na wawili na wafwasi makumi saba ambao hesabu yao ilijulikana vizuri. Munaona? Lakini shetani anaweza tu kudanganya yule aliye zaliwa kwa kudanganywa. Kwani Biblia inasema kwamba ingewezekana, wateule wange weza kudanganywa lakini haiwezekani! Mungu ni mwema na katika wema wake, ataruhusu siku moja maganda ya upofu ianguke toka macho yetu [*Kusanyiko wanasema: "Amina!"*]. Wanaomba wapelekwe mbele ya kiti cha enzi cheupe lakini kwa wale waliyo amini ujumbe ya wakati yao, hawatafika hukumuni, tayari wamehukumiwa kupitia kusulibiwa kwa Yesu-Kristo. Musa atakuwa kama mkuu wa korti ya sheria kwa wale wote waliyo kuwa kule jangwani ya Sinai, ndivyo William Branham atakuwa kwa wote waliyo ishi wakati yeye alikuwa nuru ya ulimwengu kama vile inavyo andikwa katika Yoane 9:5. Na mjumbe wa Mt.25:6 atakuwa hivyo kwa kizazi hiki.

Baada ya haya makanisa za kiinjili, ndugu za wafarisayo wakaja na kumwambia yule aliyekaa juu ya kiti cha enzi: *"Sisi ni wa Yesu, hatukumwamini mwingine ila tu Yesu!"* Lakini Bwana atawaambia: *"Muliwepo Israeli nilipo kuwa duniani? Nilipo kuwa duniani, niliwaambia hata mitume wangu wasikwende kwa watu wa mataifa kwani huduma yangu ilikuwa tu kati ya ndugu zangu wayahudi, basi namna gani ninyi, muliyo watu wa mataifa, munasema: Sisi ni wa Yesu, tulikuwa wafwasi wako duniani?... Je! Sikuwaahidia nyota saba ambao ni malaika saba mulilazimishwa kuwasikiliza ili muokolewe? Sababu gani hamukuwasikiliza? Ondokeni mbali nami, watenda maovu!"* munaona? Yesu alisema*: "Je! Sikusema katika Yoane 9:5 kwamba: «WAKATI NINGALI duniani, mimi ni nuru ya ulimwengu» na hivyo, Yoane alikuwa nuru ya ulimwengu kabla yangu mimi* [Yne.5:35] na wakati sitakuwa tena duniani kutakuwa wengine duniani watakao kuwa nuru ya ulimwengu kwa kuwaangaza kama vile Paulo?" Munaona? Kinywa yao itafungwa!

Na papa wa… msimamizi wa kanisa la pentekoste atakaribia akisema: *"Bwana, mimi ni mtume Yao Bio, nilifanya miujiza nyingi kwa jina lako"* Bwana atamwambia: *"Wewe ulikuwa mtume wa mjumbe wangu gani?"* Atasema: *"Bwana, nilikuwa mwenyi busara, sikuamini mtu mwingine ila wewe tu, nilikuwa mtume wa Injili yako"*. Bwana atamwambia: *"Mitume wangu walikuwa kumi na wawili, wewe ni wa wapi?"* [Kusanyiko inapaza sauti: "Amina!", ndgu filipo anasimama kidogo]… Na mkuu na mwenye heshima kuu mtume Yao Bio, msimamizi wa kanisa la pentekoste, akafungwa kinywa na Bwana akasema: "mumfunge na mumtupe nje, mahali kutakuwa kulia na kusaga meno. Je! Sikuwaambia kwamba wakati imekuja ambapo kuabudu itakuwa katika Roho na kweli na kwamba si lazima tena kutazamia Israeli. Je! Sikuwaambia kwamba nitatembea kati ya mataifa katikati ya taa saba za dhahabu? Je! Sikuwaambia kwamba sawa sawa umeme unatoka mashariki hadi magharibi, ndivyo nitajifunua kwenu? Na wakati Paulo alikuwa kazini huko mashariki, je! Haikuwa ni mimi? Na Antipasi [Ufu.2:13] alipo kuwa kazini, je! Haikuwa mimi? Na mtumishi wangu Martin alipo kuwa kazini huko Ufaransa, je! Haikuwa mimi? Na Kalvini alipo kuwa kazini huko Usuisi, je! Haikuwa mimi? Na wakati Yoane Huss, mtakatifu Patrick, John Wicliff,… walikuwa kazini, je! Haikuwa mimi? Na Lutheri alipo kuwa kazini huko Ujerumani, je! Haikuwa mimi? Na Wesley alipo kuwa kazini, je! Haikuwa mimi? Na William Branham alipo kuwa kazini, je! Haikuwa mimi? Na Mt.25:6 ilipo timia, haikuwa mimi? Kwa nini hamukuwaamini? Kama vile nilituma Elia, Yeremia, Habakuki, Agai, Hosea, Zakaria, Amosi, Sofonia, Isaya,… kwa wayahudi, ndivyo hivyo, kwenu pia, niliwatuma hao kufwatana na ahadi ya Mt.23:34 na muliwakataa! Ondokeni basi karibu nami, munao tenda uzalimu! [Kusanyiko wanapaza sauti kwa furaha, ndugu Filipo anasimama tena kidogo!]…ikiwa hapa kuna ndege asiye tai, abaki kimia kwani tai wanakuwa mezani. [*Kusanyiko linapiga kelele: "Amina!"*]. Sisi ni samaki, tulizaliwa samaki na hatuwaombe kaa za pwani kugeuka samaki kama sisi!

Munaona? Mtu anasimama na kujenga dhehebu ya kidini ambayo anaita: kanisa na kujidai kuwa mtume, mchungaji, mwalimu, injilisti au mfwasi…siyo wa nabii mjumbe wa wakati wake lakini wa Yesu mnazareti ambaye hakumjua na watu wanamfwata kama wanyama. Munaona? Japo ni desturi ya zamani ya upagani. Ninataja tu mifano miwili: nitasoma maneno fulani ambayo…[Ndugu Filipo anatafuta ukurasa]… mnisamehe!... ndiyo! Ni hapa! Ni Daniel-Rops, *Historia ya kanisa la mitume*, ukurasa…ukurasa 157 ninasoma: *"Na kaizari Kostantino alipo ona kwamba mwisho wake unakaribia, akajengesha kanisa kubwa kwa heshima ya mitume watakatifu inayo sanduku kumi na mbili za mawe ya damani kwa ukumbusho wao na ya kumi na tatu iliyo tayarishwa kwake"*. Na munajua kwamba kanisa kuu na ya ajabu ulimwenguni yapatikana katika Côte d'Ivoire ikiwa na sanamu ya kumi na tatu, ile ya Houphouët Boigny, inayo wakilisha mtume wa kumi na tatu wa Yesu. Munaona? Kama Kostantino na Houphouët, nyinyi ni huru kuendelesha hesabu ya wafwasi na mitume wa Yesu kama vile babu zenu pia walijifanya wafwasi wa Musa kuliko wakubali Yesu wa Nazareti, nuru ya wakati yao. Ikiwa Mungu ataokoa moja wenu au moja wa wale wanao wafwata, itamubidi kuwaomba wafarisayo msamaha na kuwaokoa wote hata Yuda vilevile! Lakini tunajua ya kwamba Mungu hawezi kamwe kutuma kanisa duniani lakini Ujumbe na wanao toka katika madhehebu kwa kukusanyika kando ya huu Ujumbe wao ndiyo wanaunda Kanisa. Lakini kwanza Ujumbe, jambo mpya ambalo dunia haikulijua na linakuja kama nuru ya ulimwengu. Munaona? Na Musa, alileta sheria, na kila nabii… hapana sinagogi lakini Ujumbe uliyo katika kitabu moja. Hamutaona kamwe kanisa au sinagogi la nabii fulani lakini Ujumbe moja…

Munaona, Wesley atawaambia walutheri waliyo kataa Ujumbe wake: « *Musifikiri kwamba mimi, nitawasitaki mbele ya Baba ; kuna moja anaye wasitaki, Lutheri ambaye munamtumainia*» [*Kusanyiko wanasema: Amina!*]. William Branham aliweza kuwaambia wamethodisti: « *Musifikiri kwamba mimi, nitawasitaki mbele ya Baba ; kuna moja anaye wasitaki, Wesley ambaye munamtumainia*» [*Kusanyiko wanasema: Amina!*]. na mimi ninaweza kuwaambia wabranhamisti: « *Musifikiri kwamba mimi, nitawasitaki mbele ya Baba ; kuna moja anaye wasitaki, William Branham ambaye munamtumainia*» [*Kusanyiko wanasema: Amina!*]. Munaona? Hukumuni, wabranhamisti waliyo sikia kelele ya katikati ya usiku na wakaikataa walikuja na ilikuwa tu hivi. Ni Neno la unabii! Ikiwa wewe uliishi kwa mwaka 2002, wewe ni chini ya utawala wa Mt.25:6. Uwe mkatholika, protestanti, wa kiinjili au branhamisti, jua kwamba kama Mungu ndiye alinipa Ujumbe huu… Kama vile Isaya na Yeremia, yule aliyewahukumu duniani tangu 2002 atakuwa mwamuzi wenu mbele ya Mungu. Wafarisayo walikokota gombo ndefu kwenyi kiti cha hukumu na wakasema: "*Sisi ni wa Musa,*… leo wangeliweza kusema: *Sisi ni wa Yesu*!" [*Kusanyiko linasema: Amina!*] ni pale wengine kati ya wabranhamisti walikuja mbele ya kiti cha hukumu! Walisema: *"Bwana, Hatukukataa Kelele ya katikati ya usiku, lakini kwa hadhari, tulingoja uthibitisho ili tujiunge nao…"* Na Bwana atawaambia: "Ninyi munao Ujumbe wa jioni mulingoja nini??? Uthibitisho!!!… *"Bwana, hukumthibitisha William Branham kwa nguzo la moto?"*… Uthibitisho gani uliruhusu kukubali Yeremia, Isaya, Hagai, Hosea, Yoeli, Danieli, Sofonia, Habakuki… Lutheri, Wesley, na wengine? Mulingoja Uthibitisho ijapo makahaba wa kibatisti, methodisti, katholika, pentekoste waliingia??? Je! Mimi nanyi tulisaini mapatano ya Uthibitisho??? Je! Biblia inasema kwamba nililazimishwa kufanya vile??? Ondokeni kwangu na nendeni katika moto iliyo tayarishwa kwenu kabla dunia kuumbwa!!!". [*Kusanyiko linasema: Amina!*]. Na ni William Branham mwenyewe ndiye akawahukumu mbele ya Mungu kama alivyo andika Yoane 5:45! Unapo kataa Ujumbe ya wakati yako, ni mwisho kwako!!! Na mafungo yako na maombi yako ni machukizo [mbele ya Mungu]! Bidii yako, matunda yako ya Wagalatia 5:22 ni machukizo na juu ya yote, Yesu wako ni shetani. [*Kusanyiko linasema: Amina!*].

Na wakati nabii mjumbe anapo kuwa akihubiri, kila mchungaji, mwalimu, nabii, injilisti au mtume asiye chukua ujumbe wake yeye ni wa shetani. Munalazimishwa kuwa sauti ya Ujumbe wake kama sivyo shetani ndiye munatumikia. Noa alipo kuwa akihubiri, hungeweza kutumikia Mungu ila tu kama wewe unaleta watu kuamini Ujumbe wa Noa. Yeremia alipo kuwa akihubiri, hamunge weza kutumikia Mungu katika masinagogi zenu ila tu kwa kuwaleta watu kuamini maneno yaliyosemwa na Yeremia. Yesu alipo kuwa akihubiri, hungeweza kutumikia Mungu ila tu kwa kuwaleta watu kufwata Ujumbe wa Yesu. Amosi alipo kuwa akihubiri, Mungu hangeweza kukubali ukuhani wa Amazia ila tu kama yeye pia alimkubali Amosi kwani Biblia inasema katika Yoane 6:28 kwamba… tuisome: « *Basi wakamwambia: Tufanye nini kwa kufanya kazi ya Mungu? Yesu akajibu akawaambia: Hii ndiyo kazi ya Mungu, mumuamini yule aliyetumwa na Mungu*». Munaona? Huwezi kumtumikia Mungu ila tu kwa kuamini yule aliye tumwa na Mungu. Aliye na masikio kwa kusikia, asikie!

MAWASILIANO: Ndugu Kacou Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org